*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*____________________

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI**

**021** **KISWAHILI**

**Muda: 2:30** **Mwaka: 2025**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi (10)**.
2. Jibu maswali **yote** kwenye nafasi ulizopewa.
3. Sehemu A na C zina alama **kumi na tano (15)** kila moja na sehemu B ina alama **sabini (70)**.
4. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.
6. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha upimaji.
7. Andika **Namba yako ya Upimaji** katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAHIHI YA MTAHINI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAHIHI YA MHAKIKI** | | |

2 519021 100012



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi* ____________

## SEHEMU A (Alama 15)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika vipengele (i) - (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Mpangilio sahihi wa maneno yafuatayo katika kamusi ni upi?
- A Shaba, shadidi, shahada, shamba, shangazi
- B Shaba, shahada, shangazi, shamba, shadidi
- C Shaba, shangazi, shamba, shadidi, shahada
- D Shaba, shamba, shangazi, shadidi, shahada

(ii) Mwalimu alitufundisha kuwa mizani ni kipengele muhimu cha fani katika ushairi wa fasihi simulizi. Ipi ni maana sahihi ya kipengele hicho?
- A Silabi au sauti zenye milio ya kufanana katika ubeti
- B Mstari mzima wa shairi unaojitosheleza kimaana
- C Mshororo wa mwisho wa kila ubeti wa ushairi
- D Idadi ya silabi katika mshororo au mstari wa shairi

(iii) "Wanafunzi hawapendagi somo la Hisabati kwa kuwa ni gumu." Kosa la kisarufi lililopo katika sentensi hiyo limesababishwa na nini?
- A Kutozingatia alama za uandishi
- B Uongezaji wa kiambishi
- C Udondoshaji wa herufi
- D Upatanisho wa kisarufi

(iv) Sentensi ipi imejengwa na kauli ya kutendewa?
- A Shamba limelimika lote
- B Kitabu kimechanika
- C Mafuta yameisha kabisa
- D Nyumba imejengewa ua

(v) Miundo ya barua ya kindugu na rasmi hutofautishwa na jambo lipi?
- A Anwani ya mwandishi
- B Tarehe ya barua
- C Anwani ya mwandikiwa
- D Jina la mwandishi

(vi) Sentensi ipi **si sahihi** kuhusu sifa za fasihi simulizi?
- A Huwasilishwa kwa mdomo
- B Huwa ni mali ya jamii nzima
- C Hubadilika kulingana na wakati
- D Humilikiwa na mwandishi

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(vii) Sentensi ipi haina kielezi cha mahali?
A Anasoma kwa bidii
B Anapikia chai jikoni
C Anachezea uwanjani
D Dereva ameingia barabarani

(viii) Nyenzo kuu ya ufahamu wa kusikiliza ni ipi?
A Kusoma matini kwa makini
B Kutambua aina ya matini
C Kusikiliza matini kwa makini
D Kujibu maswali kwa makini

(ix) Maelezo yapi yanabainisha udhaifu wa kuhifadhi kazi za fasihi simulizi kwa njia ya kichwa?
A Haihitaji gharama
B Huwasilishwa popote
C Humilikiwa na hadhira
D Hupotea kwa urahisi

(x) Sehemu ya neno inayoundwa na konsonanti na irabu au irabu peke yake na hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti huitwaje?
A Sauti B Silabi
C Neno D Sentensi

2. Oanisha viambishi vilivyopigiwa mstari katika **Orodha A** na dhima ya kiambishi husika kutoka **Orodha B** kisha andika jibu sahihi katika kisanduku ulichopewa.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Ali<u>cho</u>kimbia | A Kiambishi awali cha nafsi ya pili umoja |
| (ii) <u>Ha</u>kuja | B Kiambishi cha usababishi |
| (iii) Ni<u>na</u>umwa | C Kiambishi awali cha nafsi ya tatu umoja |
| (iv) Pig<u>isha</u> | D Kiambishi tamati cha kutendwa |
| (v) <u>U</u>liumia | E Kiambishi awali cha ukanushi |
| | F Kiambishi awali cha urejeshi |
| | G Kiambishi awali cha njeo |

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | | | | | |

Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU B (Alama 70)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:

Wananchi wa Tanzania tunalo jukumu kubwa la kulijenga taifa letu. Tukumbuke kuwa tunapolijenga taifa letu tunawajenga watu wake, kwa kuwa taifa ni jumuiya ya watu. Kuna njia moja muhimu inayoweza kutumika ili kuwafanya watu wajiletee maendeleo yao wenyewe ambayo ni kuelekezwa na kuzingatia maelekezo sahihi ya viongozi wao. Uongozi wa jambo lolote huzingatia kuzungumza na kushauriana na watu, kuwaeleza na kuwashawishi.

Katika nchi ya Tanzania, mazungumzo, ushauri, maelekezo na vishawishi baina ya viongozi na watu katika kuleta maendeleo na kulijenga taifa yanafanyika kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili kwa hivi sasa kimekuwa chombo **adhimu** kinachotuwezesha kupeana maelekezo na kutoa mrejesho wa maelekezo yaliyotolewa.

Kiswahili kimekuwa mstari wa mbele katika kazi kubwa ya kulijenga taifa letu. Ili kazi hii ifanikiwe yatubidi wananchi wote wa Tanzania tujifunze Kiswahili, tukiheshimu na tukitumie katika shughuli zetu zote. Ikiwa **tutakibeza** na kuamua kwamba kila mmoja wetu ashikilie lugha ya kabila lake, basi **yatatukumba** matatizo ya ukabila.

Tuangalie nasi tusije tukashindwa kuendelea kujenga nchi yetu kwa sababu ya kukosa maelewano. Kama hatuna lugha ya kutuunganisha tutashindwa kutekeleza majukumu tunayopewa na viongozi wetu, ukiwemo utii wa sheria na kutimiza mipango mbalimbali. Kukosa maendeleo si shabaha yetu, hivyo, jambo kubwa la kwanza yatupasa tufahamu kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya taifa tusifanye **ajizi** tunapaswa kuitumia.

**Maswali**

(a) Andika kichwa cha habari uliyosoma kwa maneno yasiyozidi matano.

______________________________________________

______________________________________________

(b) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika habari uliyoisoma:

(i) Adhimu______________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(ii) Tutakibeza___________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

***Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*** ____________________

(iii) Yatatukumba ____________________

____________________

____________________

(iv) Ajizi ____________________

____________________

____________________

(c) Ni njia ipi inashauriwa kutumika katika kuwaletea watu maendeleo?

____________________

____________________

____________________

(d) Fupisha habari uliyosoma kwa maneno yasiyopungua 50 na yasiyozidi 60.

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

4. Kwa kutumia mifano, fafanua tofauti ya msingi iliyopo katika jozi zifuatazo za maneno:

(a) Kivumishi na kiwakilishi

(b) Kitenzi kikuu na kitenzi kisaidizi

(c) Kihisishi na kiunganishi

(d) Nomino dhahania na nomino za pekee

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(e) Vielezi vya wakati na vielezi vya mahali

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

5. Eleza dhima moja kwa kila kiambishi kilichopigiwa mstari katika maneno yafuatayo:

(a) Hapig<u>i</u>

______________________________

(b) A<u>na</u>ondoka

______________________________

(c) Wali<u>ku</u>ona

______________________________

(d) Shik<u>ik</u>a

______________________________

(e) <u>M</u>tu

______________________________

(f) <u>Vi</u>ambishi

______________________________

(g) <u>Ha</u>wapo

______________________________

(h) <u>Wa</u>takuja

______________________________

(i) <u>Hu</u>endi

______________________________

(j) O<u>an</u>a

______________________________

6. Bainisha kosa lililopo katika tungo zifuatazo kisha ziandike tungo hizo kwa usahihi. Kipengele cha (i) kimetumika kama mfano.

(i) Huyu ni lafiki yangu.

Kosa: lafiki

Tungo sahihi: Huyu ni rafiki yangu.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ii) Rete hicho kitabu.

__________________________________________

__________________________________________

(iii) Mimi ni mwanainji wa Tanzania.

__________________________________________

__________________________________________

(iv) Mama anakaaga jikoni anapopika.

__________________________________________

__________________________________________

(v) Mutu huyu anaumwa.

__________________________________________

__________________________________________

(vi) Nipe fiatu nivae.

__________________________________________

__________________________________________

7. Eleza kwa kifupi namna njia zifuatazo za mfumo wa mawasiliano zinavyokidhi mawasiliano katika jamii.

(a) Mdomo

__________________________________________

__________________________________________

__________________________________________

(b) Magazeti__________________________________

__________________________________________

__________________________________________

__________________________________________

(c) Redio

__________________________________________

__________________________________________

__________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(d) Simu ya mkononi

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(e) Televisheni

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

8. (a) Kamilisha methali zifuatazo:

(i) Kuishi kwingi ______________________________

(ii) ______________________________ hula na wa kwao.

(iii) ______________________________ huvikwa pete.

(iv) Asiyekubali kushindwa ______________________________

(v) Jambo usilolijua ______________________________

(b) Taja njia tano zinazotumika kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.

(i) ______________________________

(ii) ______________________________

(iii) ______________________________

(iv) ______________________________

(v) ______________________________

9. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata.

Jembe wangu nakuhitaji, uje unipe neema,
Jembe wewe ndiwe chaji, twakuenzi tangu zama,
Jembe wewe ni mpaji, wa baba na hata mama,
Jembe ndiwe mkombozi, tangu enzi za wahenga.

Jembe wewe wasifika, humtupi mkulima,
Jembe shamba tukifyeka, nawe wafanya kulima,
Jembe yakija masika, nawe nyuma himahima,
Jembe ndiwe mkombozi, tangu enzi za wahenga.

Jembe pengi umefika, ukweli tunausema,
Jembe kwetu ukifika, tunapata usalama,
Jembe njoo pasi shaka, kisha tujipatie mtama,
Jembe ndiwe mkombozi, tangu enzi za wahenga.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**Maswali**

(a) (i) Shairi hili lina muundo gani?

(ii) Bainisha kituo bahari katika shairi hili.

(b) Eleza dhamira kuu ya shairi hili.

(c) Jembe limepewa uwezo wa binadamu wa kutenda au kufanya jambo. Tamathali gani inayotumika katika fasihi yenye sifa hiyo?

(d) Neno "zama" ni sawa na neno gani katika shairi hili?

(e) Eleza falsafa ya mtunzi wa shairi hili.

**SEHEMU C (Alama 15)**

Jibu swali la **kumi (10)**.

10. Wewe ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Chaijaba S.L.P 207, Morogoro na unatarajia kufanya kazi ya kuuza magazeti katika likizo yako ya Desemba mwaka huu. Andika barua kwa Mkurugenzi Mtendaji wa gazeti la Nipashe, S.L.P 1012, Dar es Salaam kuomba kazi hiyo. Jina lako liwe Shukuru Maarifa.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*** ____________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*____________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org